www.arena.co.ke 0713779527

DARASA LA SABA

LUGHA: MUHULA WA KWANZA

Ufahamu: sauti ya ukimwi

Kuchambua picha kwenye ufahamu

Kusoma ufahamu kwa kutumia mbinu ainati

Kuchambua maudhui

Kutambua na kujadili misamiati kwenye ufahamu

Kueleza maana ya misamiati

Kutunga sentensi kwa kutumia misamiati

Sarufi: matumizi ya ‘kwa”

Ni kiambishi ambacho hutumika kuleta dhana mbalimbali

Kwa inafaa itumike ipasavyo

Usitumie kwa kama kihusishi cha mahali kama vile kwa duka

Mifano

KKD UK 80-82

MUFTI UK 98-100

KURUNZI UK 134

Kusikiliza na kuongea: nyimbo

Ni mbinu ya kuyapanga maneno ili yawe na sauti ya urari

Nyimbo huwa na nasaha, ujumbe, wazo au mafunzo Fulani

Nyimbo zisipotumika vizuri huweza kuvuruga maadili, heshima na usawa katika jamii

Mufti uk 102-103

Kuandika: hati nadhifu

Hati ni muhimu katika uandishi

Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi mara kwa mara ili aboreshe hati yake

www.arena.co.ke 0713779527

Azingatie miundo ya herufi mbalimbali

Anakili au asikilize maneno sentensi au aya mbalimbali

Msamiati: vitawe

Vitawe ni maneno yaliyo na maana zaidi ya moja

Hutokana na neno tawi

Neno moja linaweza kutumiwa kuleta maana tofauti na nyingine

Mfano

Somo - mpango wa mafundisho ya elimu

Mtu wa jina moja na mwengine kunga unyogoni

Asilia

Kurunzi 7 uk 19-20

Mufti 7 uk 104

Kkd 7 uk 75

Kusoma: maktaba

Maktaba ni mahali maalum ambapo vitabu huhifadhiwa

Vitabu hivi huwezwa kugawanywa kulingana na malengo, matumizi na viwango vya wasomaji

Vinaweza kuwa ni vya handithi, vitendawili, mashairi na mazoezi

Mwalimu atenge muda maalum ili mwanafunzi awe na uzoefu wa kusoma

Asilia

Kurunzi uk 72-73

Mufti uk 106

Sarufi: mnyambuliko wa vitenzi

www.arena.co.ke 0713779527

Huku ni kuvibadili vitenzi kwa kurefusha viambishitamati ili kuleta kauli mbalimbali

Kauli hizi ni

Tendana: uma - umana

Tendesha: lala – laza

Tendeka: Lima – limika

mwanafunzi sharti atumie kamusi sahii kwa marejeleo

Asilia

Mufti uk 106-108

Kurunzi uk 20 – 21

Kusikiliza na kuongea: shairi

Ni tungo wa kisanaa unaozingatia kanuni au arudhi za ushairi

Arudhi hizi ni kama

- Idadi ya silabi
- Vina
- Mishororo
- Beti

Shairi huwa na ujumbe mafunzo na maudhui

Lazima liwe na urari na mtiririko wa mawazo

Mufti uk 109

Kurunzi82-83

Kuandika: sentensi

Sentensi ni mpangilio wa manenoili pawe na mtiririko na mshikamano mwafaka

Kuna sentensi za aina mbalimbali

Mwanafunzi aweze kutunga sentensi kwa kufuata mpangilio unaofaa

Mufti uk 110

www.arena.co.ke 0713779527

Msamiati: tarakimu

Ni herufi za hesabu zinazoonyesha idadi Fulani

Mwanafunzi aweze kujua tarakirimu zaidi ya milioni moja na akipewa maneno aweze kuandika

Mufti uk 111-112

Kurunzi uk 112-113

Kkd uk 68-69

Ufahamu: matibabu

Kuchambua na kutaja yaliyomo katika mchoro

Kusoma ufahamu kwa kutumia mbinu ainati

Kutambua misamiati na maana yake na kutunga sentensi sahihi

Kuchambua maudhui

Mufti uk 114-117

Sarufi: mnyambuliko wa vitenzi

Kurejelea kauli mbalimbali za mnyambuliko hasa kauli ya kutendesha

Wanafunzi wataje vitenzi mbalimbali vinavyowatatanisha

Mwalimu asisitize kuhusu kauli ya kutendesha

Mufti uk 117

Kkd uk 92

Kusikiliza na kuongea: methali

Ni aina ya semi

Ni mtungo wa maneno wenye maana fiche

Mwanafunzi aweze kujua jinsi ya kukamilisha methali alizopewa

Mfano

Macho hayana _____

www.arena.co.ke 0713779527

Chovya chovya humaliza _____

Kitanda usichokilalia _____

Mufti uk 103

Kkd uk 117

Kuandika: imla

Imla humpa mwanafunzi mazoezi ya tahajia, uakifishaji, usikivu wa kina na hati bora

Mwanafunzi atasomewa maneno na sentensi na mwalimu

K k d uk 82

Msamiati: utaifa

Ni majina ya watu yanayoonyesha uhusiano uliopo baina ya watu nanchi zao

Kuna watu walio na majukumu, mitazamo na uhusiano wa aina mbalimbali

Uhusiano huu unaweza leta matokeo hasi au chanya

Mfano

Mlowezi – anayehama nchi nyinginena kukaa huko

Mzalendo – anayependa nchi yake kwa dhati nay u tayari kuitetea

Mufti uk 119-120

Kurunzi uk 78 k k d uk 77

Ufahamu: jinamizi la sukuma wiki

Kuchambua picha vitabuni

Kusoma ufahamu kwa ufasaha

Kuchambua maudhui na msamiati uliotumika

Kutunga sentensi kwa kutumia msamiati uliopewa

Mufti uk 122-123

www.arena.co.ke 0713779527

Sarufi: tanakali za sauti

Ni maneno yanayoonyesha au kuiga milio ya sauti, hali Fulani, sura au vitendo mbalimbali

Hutumia kusisitiza namna vitendo vilivyo, vinavyotendeka au kitakavyotendeka

Mfano

Funika gubigubi!

Papatika papatupapatu!

Kula fyu!

Kuregea regerege!

Mufti uk 124-125

K k d uk 117-118

Kusikiliza na kuongea: hotuba – zimwi la ukumwi

Wanafunzi wasome makala na kuelewa

Wachambue ujumbe uliomo kwenye makala

Wajifunze mambo muhimu

Mufti uk 125-127

Kuandika: mashairi

Mwanafunzi ajue arudhi zote za shairi

Azitumie arudhi hizo kutungia mashairi ya tathlitha na tarbia

Mufti uk 127

K k d uk 149

Msamiati: vitawe

Ni maneno yaliyo na maana zaidi ya moja

Mifano

Mbuzi – mnyama mdogo wa nyumbani

www.arena.co.ke 0713779527

Chombo au kifaa cha kukunia nazi

Mwalimu aorodheshe vitawe zaidi

Mufti uk 127-128

Ufahamu: chuki

Kuchabua mchoro kwenye vitabu

Kusoma na kuuelewa ufahamu

Kuchambua ujumbe mkuu, msamiati na tamathali zilizotumiwa

Kutunga sentensi wakitumia misamiati

Mufti uk 130-132

Sarufi: matumizi ya vihusishi 'katika' na kiambishi tamati –ni'

Katika na –ni ni vihusishi vinavyotumiwa kumaanisha ndaniya

Vihusishi hivi havitumiwi pamoja katika sentensi

Mfano

Ingia katika darasani ni kosa

Ingia darasani au ingia katika darasa ni sahihi

-ni huambishwa kwenye nomino za kawaida kisha nomino hiyo huorodheshwa katika ngeli ya PAKUMU

Katika hutumiwa kuleta maana ya

Miongoni mwa

mtu mmoja katika wale ni mgonjwa

wakati

Tutakuwa na likizo katika mwezi wa Aprili

Ujumla wa vitu

Wote walishiriki katika michezo hiyo

www.arena.co.ke 0713779527

Mufti uk 132-134

K k d uk 122

Kusikiliza na kuongea: mchezo wa kuigiza

Ni hali ya kusema, kutenda na kuonyesha matukio kwa njia ya sanaa

Vitendo, milio na sauti na mavazi hutilia mkazo yale yanayoigizwa

Lengo huwa ni kutoa funzo Fulani

Mufti uk 135-139

Kurunzi uk 84-85

Kuandika: handithi fupi

Wanafunzi waandike handithi fupiwakirejelea mchoro

K k d uk 144

Msamiati: tarakimu 5,000,000-6,000,000

Wanafunzi waweze kuandika tarakimu kati ya 5,000,000 – 6,000,000 kwa maneno na nambari

Sharti waweze kutumia maneno kama laki, milioni , elfu

Uakifishaji mwafaka utumiwe

Mufti uk 139-140

Ufahamu: ufundi wa insha

Kuchambua picha vitabuni

Kusoma ufahamu kwa ufasaha

Kutaja na kuorodhesha misamiati na maana yake

Wanafunzi watunge sentensi wakitumia misamiati

Wajibu maswali

www.arena.co.ke 0713779527

Mufti uk 142-144

Sarufi: alama za uakifishaji

Ni alama zinazotumiwa ili kuwasilisha nia halisi na maana kamili ya kwenye maandishi

Alama hizi pia hufanya kusomeka kwa sentensi kuwa rahisi

Mfano

Nusukoloni /semikoloni/nukta kipumuo ;

Hutumiwa kuunganisha mawazo mawili

Mfano

Ninataka kuondoka mapema ;sipendi kuchelewa

Koloni/nuktambili/nukta pacha :

Hutumiwa kuonyesha orodha ndefu

Mfano

Nenda ununue vutu vifuatavyo:maziwa, mkate, sukari, mafuta na chumvi

Mufti uk 144-145

Kurunzi uk 123-125

Kusikiliza na kuongea: makala

Kusoma makala kwa kina

Kuelewa ujumbe mkuu

Kujadili kuhusu mbinu bora za kuepuka kuathirika na manbo yanayochangia kuzorota kwa maadili

Kutaja vyombo vya kisasa vinavyochangia kuzorota kwa maadili

Mufti uk 145-146

Kuandika: imla

Kuandika maneno yenye sauti f, v, l, r, g, k

www.arena.co.ke 0713779527

Wasikilize maneno kwa umakinifu ili wayaandike kwa usahihi

Watunge sentensi eakitumia maneno hayo

Msungi uk 133

Msamiati: viwandani

Viwanda ni mahali ambapo bidhaa, vitu, mashine na vipuri mbalimbali huundiwa

Huwa na mitambo mbalimbali

Mitambo na mashine hurahisisha kazi

Mifano

Fuawe

Chombo cha mhunzi anachowekea chuma anachokifua

Kreni/kirini

Mashine nzito ya kuinulia mizigo mizito hasa bandarini

Mufti uk 147-148

Tujivunie uk 120-121

Shairi: daladala

Wanafunzi waelewe kanuni za ushairi

Walighani shairi walilopewa

Kuuchambua ujumbe katika sentensi hiyo

Kuchambua msamiati uliotumiwa

Kujibu maswali yaliyotolewa

Mufti uk 150

Sarufi: ukubwa, udogo na wastani wa nomino

Ukubwa ni hali ya kukuza nomino na udogo ni hali ya kudunisha nomino

Wastani ni hali ya kawaida ya nomino

www.arena.co.ke 0713779527

Nomino katika ukubwa huwekwa katika ngeli ya LI – YA na nomino katika hali ya udogo huwekwa katika ngeli ya KI – VI

Zipo kanuni ambazo hutumiwa

Noino zenye silabi mbili- dodosha moja

Mtu- jitu

Nomino zinazoanza kwa ki dondosha ki pachuka ji

Kiatu – jiatu

Mufti uk 151-152

K k d uk 132, 148

Kusikiliza na kuongea:shairi – ngonjera

Wanafunzi waweze kuigiza shairi walilopewa

Kuchambua ujumbe uliomo

Kueleza aina ya shairi na msamiati uliopo

Kujibu maswali

K k d uk 146

Kuandika: imla

Mwalimu awasomee wanafunzi aya kasha wandike madaftarini

Wafanye masahihisho

Tujivunie uk 17

Msamiati: viumbe vya kike na kiume

Hii ni hali ya jinsia au uana

Viumbe vyenye uhai huwa vya kike au kiume

Sharti viambatanishwe vinavyofaa

Mfano

www.arena.co.ke 0713779527

Mkewe – mumewe

Jike – dume

Halati – mjomba

Mufti uk 154-155

Kurunzi uk 69

Kusoma: makala magazetini na majarida

Kusoma makala katika vitabu

Kuchambua picha katika kitabu

Kutaja mambo muhimu katika magazeti na majarida

Tofauti kati ya majarida na magazeti ni kuwa magazeti huchapishwa kila siku lakini majarida huchapishwa baada ya muda Fulani

Kuchambua msamiati uliotumiwa

Kujadili na kujibu maswali

Mufti uk 157-158

Sarufi: sifa kutokana na vitenzi

Ni kuunda maneno yenye kivumishi au kusifu nomino kutoka kwenye viarafa

Sifa hizi huwa ni herufi kama f, v, mw

Mfano

Amini – mwaminifu

Sikia- sikivu

Tii – tiifu

Dhulumu – dhalimu

Mufti uk 158-159

Kusikiliza na kuongea: uso unasingiziwa

www.arena.co.ke 0713779527

Kusoma makala na kuelewa

Kuchambua ujumbe kutoka kwa makala

Kuchambua msamiati uliotumika na kutunga sentensi

Kujibu maswali

Mufti uk 159-161

Kuandika: imla

Kusikilia kwa umakinifu maneno yatakayosomwa

Kuandika kwa usahihi na hati nadhifu

Mufti uk 161

Msamiati:tarakimu 6,000,000 – 7,000,000

Mwanafunzi aweze kuandika tarakimu kati ya 6,000,00 – 7, 000,000

Kuweza kuandika kwa maneno na tarakimuna pia kuorodhesha milioni, laki, elfu

Mufti uk 162

Ufahamu: ajira za watoto

Kuchambua picha vitabuni

Kusoma ufahamu kwa ufasaha

Kutambua msamiati uliotumiwa na kutunga sentensi sahihi

Kujibu maswali uliyopewa

Mufti uk 164-166

Sarufi: virejeshi

Kuorodhesha ngeli mbalimbali na majina katika ngeli hizo

Kuorodhesha virejeshi pamoja na noino katika ngeli hizo

Kutunga sentensi kwa kutumia virejeshi hivyo

Mufti uk 166

www.arena.co.ke 0713779527

Kusikiliza na kuongea: vitendawili

Aina ya fumbo ambapo mtegaji analifahamu jibu

Majibu ya vitendawili yanahitaji Yule aliyetegewa aliwazie tena jawabu lake

Huanza hivi

“kitendawili” anayetega

“tega” anayetegewa

Iwapo atashindwa kupeana jawabu sahihi sharti apeane mji Fulani

Mfano

Kuku wangu katagia mibani – nanasi

Ajilinda bila silaha – kinyonga

Mufti uk166

K k d uk 88

Kuandika: methali

Kuorodhesha methali mbalimbali na kutumia majina kutunga sentensi

Mfano

Ganda – ganda la muwalajana, chungu kaoana kivuno

Kiatu – baniani mbaya kiatu chaje dawa

Mufti uk 103

K k d uk 167

Msamiati: watu na kazi zao

Watu hufanya kazi mbalimbali

Ni sharti tuheshimu kila aina ya kazi

Mfano

Kungwi – anayefundisha kunga za nyumbani

www.arena.co.ke 0713779527

Haali – hubeba mizigo kwa malipo

Mufti uk 167-169

Ufahamu: mawasiliano ya kisasa

Kutazama na kuchambua picha vitabuni

Kuvitambua vifaa hivyo

Kutambua ujumbe uliomo katika ufahamu

Kutunga sentensi na misamiati iliyotumika

Mufti uk 172-174

Sarufi: umoja na wingi

Kuorodhesha ngeli mbalimbali na vipingele vyake uhimu

Kutunga sentensi zenye vipingele hivyo katika hali ya umoja na wingi

Mfano

Kiatu kinachonuka hakipendezi

Viatu vinavyonuka havipendezi

Mufti uk 174-175

Kusikiliza na kuongea : misemo

Misemo ni aina ya semi yenye maana isiyolingana na maneno yaliyotumiwa

Mfano

Mkia wa mbuzi – mtu ovyo

Nguo imeruka- imekuwa fupi

Mufti uk 175

Kuandika : shairi

www.arena.co.ke 0713779527

Kutunga shairi kwa kufuata kanuni zinazofaa

Mufti uk 176

Msamiati: malipo mbalimbali

Ni ada zinazotozwa au kutolewa baada au kabla ya huduma wajibu au jukumu Fulani kutekelezwa

Malipo yanaweza kuwa ninfedha au kwa kitu chochote bora pawe na makubaliano

Mfano

Nauli – malipo ya usafiri

Mahari – malipo ya kuolea

Mufti 176-177

INSHA

MUHULA WA PILI

INSHA YA MASIMULIZI

Huzuni au tanzia

Huvi ni visa vinanyoleta majonzi, huzuni, simanzi, sikitiko au jitimai

Mikondo

Ujambazi/unyang'anyi/uporaji/wizi

Utekajinyara

Ujangili

Wizi wa mifugo

Ilaghai

Magendo

Ugomvi wa kijamii

Uvamizi na watu katili

Migomo

www.arena.co.ke 0713779527

Misamiati na mapambo

Mayowe – ukemi, usiahi, mayowe

Wasiwasi- jekejeke, jakamoyo, kiherehere

Kufa – kata kamba, enda ahera, jongomeo

Hasira – pandwa na mori, kuwa na tumbo joto, kama zaibaki kwenye kipimajoto

Nilinyapianyapia/nilinyatianyatia nyatunyatu

Joho la kiwewe lilinivaa_____

Nilichana mbuga/nilitifua vumbi ili kuyaokoa maish _____-

Moyo ulinidwikadwika/ulinipapa kama ngoma za mahepe

Malaika yalinisimama wima

Tulisikia sauti zilizotweta kama ___

Sikuyaamini macho nilipoona

Nilipiga usiahi ambao ungewafufua wafu _____

Ulimi uliniganda kinywani

Nililia kwa kite na imani lakini kilio si dawa

Nilitoka shoti kama

Ngeu ilimtiririka kama _____

Milio ya risasi ilitamalaki kwenye anga

Parafujo za miguu ziliregea

Macho yalinitoka pima kama _____

Nilitetemeka kama unyasi nyikanu _____

Kijasho chembamba kikaanza kunitoka

Methali

Mbwa hafi maji akiona ukoko

Damu ni nzito kuliko maji

www.arena.co.ke 0713779527

Tama mbele mauti nyuma

Unjanja wa nyani huishia jagwani

Siku za mwizi ni arubaini

INSHA YA MASIMULIZI – HISIA ZA FURAHA

Furaha hutokana na

Sherehe – harusi

Mwakampya

Kuzaliwa kwa motto

Sikukuu ya krismasi

Sikukuu ya pasaka

Mahafali – sherehe za kufuzu

Siku ya tuzo/harambee

Kutembelewa na wageni

Sherehe za kitaifa

Sherehe z asili

Msamiati na mapambo

Maua ya kila ainati – si asmini, mawaridi

Ukumbi ulijaa na kuwatapika adinasi

Vipaza sauti vilihinikiza sauti _____

Vyakula vya kila aina/jamii vilitishia kuangusha meza

Msichana /kidosho/kipusa alitembea kwa madaha

Mkalimani na mfawidhi walishirikiana kama

Tulilakiwa kwa kupigwa pambaja

Waja walijaa si si si si

Waja waliwasili makundimakundi/mmoja mmoja/pacha pacha

Nikitembea aste aste hadi jukwaani

www.arena.co.ke 0713779527

Kula/kushtaki njaa/fanyia mlo haki

Nilikumbuka nilivyojifunga kibwebwe/masombo

Kaka angeasi ukapera

Waja walisakata ruma/dansi

Msafara/mlolongo wa magari

Vipokezi vya methali

Yakini,_____

Waama, _____

Ama kweli_____

Wahenga hawakukosea walipokili_____

Methali

Chanda chema huvishwa pete

Baada ya dhiki faraja

Hauchi hauchi unakucha

Siku njema huonekana asubuhi

BARUA/WARAKA

Kuna aina mbili

Barua ya kirafiki

Barua rasmi

BARUA YA KIRAFIKI/KIDUGU

Huandikwa ili kupeana mwaliko, kujuliana hali, kufahamisha au kuarifu kuhusu jambo

Sehemu muhimu za barua hii ni

Anwani ya mwandishi

www.arena.co.ke 0713779527

BIDII FAULU,

S.L.P 93,

NAIVASHA.

18-11-2015

Kwa sahibu yangu, fundi msanifu ,

Utangulizi_____

Mwili

Hatima

Ni mimi wako,

www.arena.co.ke 0713779527

Jina la mwandishi

Huandikwa pembeni kabisa wa kulia sehemu ya juu

Hujumuisha jina la mwandishi au anakosomea au kufanya kazi

Huwa pia na mahali anakoishi na sanduku la posta

Kianzio

Hudhihirisha anayeandikiwa

Hubainisha uhusiano wake na mwandishi

Kwa mpendwa

Kwa laazizi

Rafiki yangu

Kwa mwanangu mpendwa

Utangulizi

Haya ni maamkizi na kujuliana hali

Mfano

Pokea salamu sufufu/furifuri

Mimi ni buheri w afya/mzima kama

Mwili

Hubeba ujumbe au kusudio la barua

Lengo/nia/azma ya kukuandikia barua hii ni _____

Ninaomba unitendee hisani/fadhila

Kwa kuwa wema hauozi

Ninakuhakikishia kuwa nitatia bidii

Ningependa kukujuvya kuwa

www.arena.co.ke 0713779527

Tumia viunganishi ili kuunganisha mawazo

Isitoshe, zaidi ya hayo, aidha

Tamati

Ningeoenda kutia nanga kwa kukueleza

Ningependa kukunja jamvi

Kwa kuwa muda umenip kisogo

Ni mimi wako mpenzi,

Ni wako mpendwa,

Jina la mwandishi

BARUA RASMI

Huandikwa ili kuwasilisha ujumbe maalum

Huandikwa ili kuomba msamaha

Kuomba nafasi kwa kazi

Kuwasilisha malalamishi

Kuagizia/kuthibitisha mapokezi ya kampuni, shirika , idara

Sehemu

Anwani ya mwandishi

Huandikwa pembeni kabisa upande wa kulia sehemu ya juu ya karatasi

www.arena.co.ke 0713779527

Hujumuisha jina la mwandishi, sanduku la posta, mahali ankoishi na tarehe baada ya anwani vuka mstari mmoja

Anwani ya mwandikiwa

Hutaja cheo cha anayeandikiwa

Taja jina la kampuni/shirika/dara

Taja S.L.P

Kianzio

Huanzia chini ya anwani ya mwandikiwa

Bwana/BW

Bibi/BI

Mabibi

Mabwana

Mtajo

Huelezea lengo la barua

Hutangulizwa kwa MINT: (mintirafu), KUH: (kuhusu), OMBI: , kumb: (kumbuka)

Pigia mstari ujumbe wenyewe

Mwili

Hubeba ujumbe wa barua

Maudhui hutegemea nia au lengo la barua

Lugha iwe rasmi

Msamiati

Nina furaha ribribi/kuu/firifuri

Nina bashasha belele

Ninasikitika ninapokuandika waraka huu ___

Ningependa kuchukua fursa/wasaa/nafasi

Kurejelea habari Fulani

Kwa mujibu w habari niliyoisoma/kutokana na taarifa/ kulingana na _____

www.arena.co.ke 0713779527

Shule.kampuni/shirika ___imesifika

Imetajwa na kutajika

Sifa zake zimeenea kote_____kamamoto nyikani kama wakati wa hari/kiangazi

Katika Nyanja za michezo ___idara/ shirika/shule yako

Wasifu/tawasifu __mimi ni mwananchi kindakindaki/halisi

Nina nidhamu na taadhima ya hali ya _____

Nina talanta katika fani ya riadha uimbaji

Nina sauti ya ninga

Nitakuwa kielelzo dhabiti kwa

Nitatia bidii za mchwa ajengaye kichunguu

Nitavumilia/nitajikaza kisabuni ili kuafikia ndoto yangu

Vyeti vyangu vimeambatanishwa pamoja na waraka huu

Tamati

Ni mwisho wa barua

Huandikwa pembeni upandr wa kulia sehemu ya chini

Herufi ya kwanza iwe kubwa

INSHA ZA METHALI

Methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiliwa na jamiina hutumiwa kufumbia jambo Fulani

Methali hutahiniwa kwa namna tatu

Ikiwa kama mada

Mwanafunzi anafaa aeleze maana ya juu na ya ndani yake na matumizi yake iwapo anaifahamu vyema

Methali za majutu, maonyo , na tahadhari

www.arena.co.ke 0713779527

Hutumiwa kuonyesha athariau madhara yanayotokea baada ya mtu kugaidi maagizo, nasaha au maonyo

Hutumiwa kutoa funzo kwa wenginekutokana na dhiki na majuto yaliyomfika mhusika

Asiyefunzwa na mamaya hufunzwa na ulimwengu

Asiyeskia la mkuu huvunjika guu

Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe

Mbio za sakafuni huishia ukingoni

Mchuma janga hula na wa kwao

Ujanja wa nyani huishia jangwani

Majuto ni mjukuu huja kinyume

Mchiba kisima huingia mwenyewe

Msiba wa kujitakia hauna kilio

Kilio si dawa

Mapambo na msamiati

Kutofuata ushauri

Alikuwa hakanywi hakanyiki

Hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini

Alikuwa haliki hatafunuki

Haambiliki hasenezeki

Alikuwa hajijui hajitambui

Kujuta

Aliishia na laiti kinywani

Alijiuma kidole/alilia chanda kili kinywani

Nilikabiliana ana kwa ana na ulimwengu usiokuwa na huruma

Niliyaona ya firauni

Nilikiona kilichomtoa kanga manyoya

www.arena.co.ke 0713779527

Kupuuza

Alivalia miwani mashauri

Niliyatemea mate mawaidha

Alijitia hamnazo

Aliyatia kapuni yota aliyoambiwa

Mambo kuharibika

Mambo yalimwendea pete/tenge/mrisi/shoto/shambiro

Kutowezekana kwa

Ilikuwa sawa na kukama tetere

Kufunuka jua kwa ungo au chekeche

Kuchota maji kwa pakacha

Tashbihi

Pukutikwa na machozi kama ngamia

Tiririkwa na machozi kama maji mlimani

Mchafu kama kilihafu/fungo

Nuka kama mzoga/beberu/kindonda

Unafiki na kujitakia shida

Chui aliyevalia ngozi ya kondoo

Panya aliyeumia na kuvuvia

Kujipali makaa kama chachandu

Kuogelea katika bahari ya moto

INSHA ZA MAELEZO

Hutoa ufafanuzi kuhusu jambo, mtu, mahali au kitu Fulani

Maelezo haya huwa ni sifa au hoja maalum

Insha hizi hutahadharisha, huelezea, huarifu na huburudisha

Mtahiniwa asijadili chini ya hoja sita

www.arena.co.ke 0713779527

Atoe hoja za ukweli

Mfano

Athari za ukimwi

Athari za dawa za kulevya

Athari za tknolojia

Mchezo ni upendao

Haki na ajira za watoto

Haki ni mstahiki au ni jambo ambalo ni halali ya mtu

Mstahiki pia ni mtu mwenye haki ya kupata kitu

Ajira ni kazi zinazofanywa katika mashamba, viwanda, nyumbani na migodini

Watoto wanapopewa ajira ni kinyume cha sharia

Baadhi ya haki hizi ni

Lishe bora

Watoto wanafaa wapewe mlo ulio na viinilishe muhimu kwa protini, kabohaidrati, madini na maji safi

Wasipolishwa huenda wakaathiriwa na magonjwa kama kwashakoo, utapiamlo

Mavazi

Humkinga dhidi ya mabadiliko ya hali ya anga

Huzuia maradhi kama mafua, nimonia na pumu

Methali

Kinga ni bora kuliko tiba

Makao salama

Humsetiri dhidi ya wanyama hatari, maadui na mabadiliko katika hali ya anga

Kupata elimu

Asibaguliwe kwa misingi ya jinsia, kidini, kikabila au rangi ya ngozi

Wasichana wasiozwe mapema

www.arena.co.ke 0713779527

Wasijiingize katika vitendo vya ukosefu na maadili kama ukahaba

Wafundishwe maadili na nifhamu

Methali

Elimu haitekeki

Elimu ni bahari

Elimu haina mwisho

Afya njema

Watoto wanafaa kukulia katika mazingira safi

Wapewe matibabu wanapougua

Wapewe lishebora

Methali

Afya ni bora kuliko mali

Kinga ni bora kuliko tiba

Wakingwe dhidi ya dhuluma

Hii ni kama kuchomwa na kukatakatwa mwilini

Waadhibiwe kwa kadiri na wastani

Wakuzwe vyema kwa maadili na mapenzi

Methali

Motto umleavyo ndivyo akuavyo

Masukuzi ya leo ndio msitu wa kesho

Wasiajiriwe

Hii ni kinyume na sharia katika katiba ya nvhi

Waajiri huwatesa na kuwanyanyasa watoto

Wengine huwarapua kwa mijeledi

www.arena.co.ke 0713779527

Wengine huajiri kama vijakazi, watwana

INSHA YA MASIMULIZI

Insha ya ndoto/njozi/ruya/ruiya

Ni aono anayoyapata mtu akiwa usingizini

Huketa hisia za furaha au huzuni

Mtu anaweza kupiga mayowe au kuweweseka kulinga na ndoto

Ndoto za huzuni zinaweza kuhusu

- Kifo
- Wizi
- Moto
- Mafuriko
- Kutishwa na viumbe hatari

Wakati mwingine mhusika hutokwa na jasho, kutabawali au kujikuta mvunguni mwa kitanda

Ndoto ya furaha humfanya mhusika kujilaumu kuwa ilikuwa ni ndoto tu

Inaweza kuhusu

- Mahafali
- Kuwa tajiri
- Kapasi mtihani
- Kuzaliwa mahali kama ikulu

Mwandishi asianze kwa kusema kuwa alianza kuota

Mapambo

Baada ya kula chajio____

Nilikuwa nimechoka hoi bin tiki_____

Niliubwaga mgogole wangu kwenye kitanda

Nilijifunika gubigubi na kulala fo fo fo

Hisia za furaha

www.arena.co.ke 0713779527

Nilifurahi ghaya ya kufurahi

Furaha upeo wa furaha

Nilidamka wanguwanguna kushika hamsini zangu

Niliamka alfajiri ya Mungu/ya musa

Ukumbi ulijaa shangwe, nderemo na hoi hoi

Nilipaa na kuelea angani

Vicheko vilishika hatamu jari moja

Hisia za huzunu – jinamizi

Maji yalikuwa yamenifika shingoni

Ulimi uliniganda kinywani

Moyo ulinipapa kama kwamba ulitaka ufunguliwe utoke

Nilishindwa kuongea ni kawa kama mja aluyepokonywa ulimi

Malaika alinisimamia tisti/wima/kititi

Mambo yaliniendea mpera mpera

Nilipiga usiahi/mayowe ambayo yangewafufua wafu

Zogo na zahama lilizuga

Nililia kwa kite na imani lakini hakuna aliyenihurumia

Niliduwaa na kubung'aa kama mzungu wa reli

Kilio cha kikweukweu kilihitimu kikawa cha mayowe

LUGHA MUHULA WA PILI

SURA YA KWANZA

Ufahamu: mpira wa midomo

Chambua picha kwenye vitabu

www.arena.co.ke 0713779527

Orodhesha msamiati na kueleza maana yake

Teua wanafunzi wasome kwa kupokezana

Wajibu maswali waliyopewa

Mufti uk 187

Sarufi: mnyambuliko wa vitenzi

Huu ni upachikaji wa viambishi kwenye mzizi wa kitenzi ili kuunda vitenzi vipya

Kauli ya kutendeshwa/fanyisha

Huonyesha kuwa kitendo kimesababishwa na kitu Fulani

Vitenzi hivi hutambulishwa na vitenzi vya, za, sha, fya, na ,sa

Mufti uk 188

Kurunzi uk 20

Kusikiliza na kuongea: sauti tata

Ziandike sentensi ubaoni

Wazima moto walikula sima kabla hawajazimia

Wafumaji walifuma sweta na sifa zao kuvuma kote kijijini

Yasome maneno yenye sauti tata huku wanafunzi wakisikiliza

Waongoze wanafunzi kutunga sentensi wakitumia maneno haya

Kamusi yaweza kutumika

Ua na hua

Zana n asana

Oga na oka

Msamiati: visawe

Ni maneno yenye maana sawa

Mwalimu atoe mifano

Shangazi – mbiomba

www.arena.co.ke 0713779527

Moto – nari

Ogopa – chelea

Kipusa – kidosho

Mufti uk 190

K k d uk 24

Ufahamu: chaurembo

Kutambua na kuchambua picha katika vitabu

Kutambua maneno magumu na kuyafafanua na kuwataka wanafunzi watunge sentensi

Wape fursa wasome na wajibu maswali

Mufti uk 193-194

Sarufi: kukanusha amri

Wakati wa amri hukanushwa kwa kutumia si

Mifani

Aende – asiende

Nimpe – nisimpe

Ule – usile

Swali lije baadaye

Wewe kunywa dawa

Wewe usikunywe dawa

Mufti uk 11-20

Kusikiliza na kuongea: handithi

Wanafunzi wataje majina ya viumbe wanavyoviona pichani

Wateuwe wasome aya kwa sauti

Wataje methali zinazohusiana na handithi hii

www.arena.co.ke 0713779527

Mtaka yote hukosa yote

Njia mbili zilimshinda fisi

Mufti uk 12

Msamiati: mapambo ya mwili

Wanafunzi wazitaje sehemu mbalimbali za mwili

Wayataje mapambo yoyote wanayoyajua

Mifano

- Kipuli
- Pete
- Ushanga
- Mkufu
- Kipini
- Hina
- Waja

Mwalimu atoe nyanzo halisi alizozichukua au michoro

Wanafunzi wataje jina la kila pambo na kutaja sehemu ya mwili linapovaliwa

Wanafunzi wasome sehemu ya msamiati na mwalimu awaongoze kwa kutoa maelezo

Wajibu maswali

Kurunzi uk 89-90

K k d uk 85-87

SURA YA PILI

Ufahamu: vituko runingani

wanafunzi kuchambua picha

orodhesha misamiati ubaoni na kutoa maana yake

wateuwe wanafunzi wsome ufahamu mmoja mmoja kwa sauti

wape fursa wasome kimya na kujibu maswali

www.arena.co.ke 0713779527

mufti uk 201-202

sarufi: wingi na kukanusha

wakati wa sasa na hukanushwa kwa ha

mifano

unasoma – mnasoma – hamsomi

unakula – mnakula – hamli

mufti uk 203

kusikiliza na kuongea: shairi

mchague mwanafunzi yeyote alikariri shairi analolijua

wapange wasome shairi hili kwa kupokezana

mwalimu aghani ubeti wa kwanza kwa sauti taratibu, mshororo baada ya mwingine

wanafunzi wajadili ujumbe katika kila ubeti

waulize maswali haya na majibu yawasilishwe kwa kuongea

shairi hili ni la aina gani?

Shairi hili lina jumla ya mishororo mingapi?

Kipokeo cha shairi hili ni?

K k d uk 70

Kurunzi uk 66

Msamiati: tarakimu 7,000,000 – 8,000,000

Anza kwa maswali ya chemsha mbongo kama

Una ywele ngapi kichwani mwako?

Kuna nyota mia,milioni au elfu ngapi angani?

Ziandike tarakirimu ubaoni ili ujue kama wanakumbuka na wajibu madaftarini mwao

6,599,790

www.arena.co.ke 0713779527

5,456,696

5,555,867

Wafanye mazoezi zaidi

Mufti uk 112

Ufahamu: kituo cha kitwea

Kuitazama picha kwa makini na kujibu maswali

Orodhesha maneno magumu ubaoni na kuyafafanua kwa kutunga sentensi

Wasome ufahamu kwa zamu na ufasaha

Wajibu maswali na kutoa majibu sahihi

Mufti uk 200

Sarufi:umoja na wingi wa sentensi

Waulize wataje majina ya ngeli mbalimbali kwa umoja na wingi

Waongoze watunge sentensi kwa kutumia majina waliyotaja

Waagize wazisome sentensi zote za mazoezi

Kusikiliza na kuongea: handithi

Anza kipindi kwa kuuliza wanafunzi walighani shairi walilolisoma hapo awali

Chambua picha kwa kina

Teua wanafunzi wasome kwa zamu na kusisitiza matamshi bora

Wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno magumu

Wajadili maswali katika makundi yao

Baada ya kujadili chukua hoja za kila kundi na kuzisoma kwa sauti

Msamiati: nomino za makundi

www.arena.co.ke 0713779527

Ni majina yanayorejelea mshikamano au mkusanyiko wa vitu au hali ya vitu hasa vya aina moja kuwa pamoja

Mifano

- Thurea ya nyota
- Halaiki ya watu
- Numbi ya samaki

Onyesha wanafunzi vifaa halisi

Watazame vifaa na wataje majina yaliyo kwa makundi

Wajibu maswali

Kurunzi uk 132

K k d uk 140

SURA YA TATU

Ufahamu: maisha ni mpango

Kuitazama picha na kutoa maelezo mafu[I kuihusu

Andika msamiati ubaoni na kutoa maana yake

Wateue wanafunzi wasome mmoja mmoja

Wajibu zoezi

Mufti uk 216-218

Kisikiliza na kuongea: mafumbo na vitendawili

Fumbo ni swali la chemsha bongo ambalo halihitaji utumizi wa akili kupata jibu sahihi

Mfano

Achora lakini hajui achoracho – konokono

Aliyekitengeneza hakukitumia, aliyekinunua hakukitumia, aliyekitumia hakukiona , ni nini?

Wafumbe na wafumbue mafumbo kwa kufuata maelekezi ya mwalimu

Kutega na kutegua vitendawili kwa kufuta maelekezi ya mwalimu

K k d uk 37

www.arena.co.ke 0713779527

Msamiati: majina ya nchi au mataifa

Wanafunzi wataje majina ya nchi jirani zinazopakana na Kenya na miji mikuu ya nchi hizo

Waongoze watahe majina ya nchi kwa kutumia ramani na wataje tafsiri yake kwa Kiswahili

Mifano

Kenya – Kenya

Ethiopia – uhabeshi

America – marekani

Waongoze wataje majina ya visiwa kama vile kisiwa cha ngazija, pemba na unguja

Wajibu maswali

Kurunzi uk 40

Ufahamu: makala, vitabu vya handithi

Vitabu hivi hupatikana maktabani

Hupatikana

Maktaba ya shule

Maktaba ya taifa

Maktaba ya nyumbani

Maduka ya vitabu

Maduka ya wamaginga

Majumba ya majirani au rafiki

Wajibu maswali

K k d uk 33

Sarufi: vivumishi vya pekee ingine na –o-ote

Vivumishi hivi ni ote, o-ote, enye, enyewe na ingine

Wape fursa watunge sentensiwakitumia vivumishi hivyo

www.arena.co.ke 0713779527

Wajibu maswali

Mufti uk 223-224

Kusikiliza na kuongea: afya na ukimwi

Ukumwi ni upungufu wa kinga mwilini

Jadili na wanafunzi mbinu za maambukizi

Epukana na yafuatayo

Ulevi wa pombe yoyote

Matumizi ya dawa za kulevya

Ukahaba na ufanyaji wa mapenzi ovyo ovyo

Kugusa damu ya mwathiriwa

Kutumia vitu kama nyembe, sindano za walioathiriwa

Wanafunzi watunge shairi wakitumia vipengele vya mjadala

Msamiati: tarakirimu 8,000,000 – 9,000,000

Wape fursa kujibu zoezi uk 225

Tarakimu ni alama ya hesabu iliyoandikwa kuonyesha idadi

Zinaweza kutumika kuonyesha nambari, miongo au hesabu

Mifano

12,000 – kumi na mbili elfu

12,002 – kumi na mbili elfu na mbili

Ufahamu: nani alaumiwe

Uchambuzi wa picha kwa muktasari

Eleza maana ya maneno magumu

Teua wanafunzi wasome kwa zamu

Wanafunzi watoe majibu kwa maswali

www.arena.co.ke 0713779527

Sarufi: vitawe

Ni maneno yaliyo na maana zaidi ya moja

Mfano

Vua- toa samaki majini

Toa nguo mwilini

Ala – aina ya mfuko ambamo kisu hufichwa

Tamko la kushangaa

Aina yoyote ya chombo cha kufanyia kazi

Ongoza wanafunzi kutoa sentensi tofauti

Kurunzi uk 19

K k d uk 75

Kusikiliza na kuongea: methali za nyuni

Ni mtungo wa sanaa ulio na maana fiche

Wanafunzi wataje methali yoyote wanayoijua

Waongoze wataje ndege yeyote wanajua

Mbuni, kuku, kipungu, kiwi

Waongoze wataje methali ambamo ndege hutajwa

Mfano

Kozi mwana mandanda kulala njaa kupenda

Maana yake ni kuwa lazima mtu mwenye uwezo wa kulitekeleza jambo autumie uwezo wake vilivyo

Mti mkuu ukigwa ndege huyumba

Maana yake ni kuwa kiongozi akitoweka waliomtegemea hutaabika

K k d uk 29

Kurunzi uk 15-17

www.arena.co.ke 0713779527

SURA YA NNE

Ufahamu: kaburi la ulevi

Uchambuzi wa picha

Waongoze wanafunzi kutaja matatizo yanayotokana na ulevi

Kutoelewana katika familia

Kuharibu kazi kwa kutoenda kazini

Ugonjwa wa ini na hata ukimwi

Eleza maana ya msamiati

Wateue wanafunzi wasome kwa kupokezana

Wajibu maswali

Sarufi: kauli ya kutendata

Kauli hii huonyesha dhana ya kurudia rudia tendo

Mfano

Kata – katakata

Imba – imbaimba

Tia – tiatia

Ruka – rukaruka

Wanafunzi wataje vitenzi mbalimbali na uandike ubaoni

Waeleze kuwa kitendo kinaporudiwa rudiwa huendelezwa kwa kwa neon moja lililoshikamana

Wajibu maswali

K k d uk 107

Kurunzi uk 20-21

Msamiati: watu na kazi zao

www.arena.co.ke 0713779527

Wanafunzi wataje watu mbalimbali kutaja kazi mbalimbali na uandike ubaoni

Wajibu zoezi A kwa kutamka kwa sauti

Wajibu zoezi B kwenye madaftari yao

Kurunzi

Uk 1-3

Ufahamu: vipawa vya kina mama

Waongoze wanafunzi kutaja majina ya watu mashuhuri wanaowafahamu kama Julius Nyerere, Nelson Mandela, Wangari Mathai

Eleza maana ya maneno magumu na wanafunzi watunge sentensi wakiyatumia

Wasome kwa zamu

Wajibu maswali

Sarufi: viwakilishi

Ni neno linalosimama badala ya nomino kama yeye, sisi, wewe

Wanafunzi wataje nomino katika ngeli mbalimbali

Waongoze kutaja viambishi nafsi kwa umoja na wingi

Eleza aina mbili za viwakilishi na utoe mifano

Wanafunzi watunge sentensi

Wajibu zoezi la mufti

Uk 240-241

Kusikiliza na kuongea: shairi – mkataa pema

Waulize wanafunzi waimbe wimbo wowote wanaoujua

Waongoze kujikumbusha mambo muhimu kuhusu ushairi

Wachague wanafunzi walighani shairi kwa sauti

Hakikisha mwanafuzi ana mwelekeo wa sauti moja katika kulighani shairi

Wajibu maswali na mwalimu aandike hoja sahihi ubaoni

www.arena.co.ke 0713779527

Kanuni za ushairi ni kama vile

Mpangilio wa mishororo

Mpangilio wa beti

Urari wa vina

Kibwagizo

K k d uk 53-54

Kuandika: misemo na vitawe

Msemo ni fngu la maneno linalotumiwa na jamii ya watu kwa namna maalumili kutoa maadili

Mwalimu arejelee kamusi ya misemo na nahau

Mifano

Kufa moyo – poteza matumaini

Kufa kikondoo – bila kulalamika

Kufa sauti – shindwa kuongea

Kurunziuk 23-24

Msamiati: tarakimu 9,000,00 – 10,000,000

Wape maswali kuhusu tarakimu walizosoma

Tumia kandi za tarakimu zikiwa nyenzo kisha mwite mwanafunzi mmoja mmoja kuchagua kadi ya tarakimu

Waongoze waandike ubaoni kwa maneno

Wajumuishe wanafunzi katika kuyatoa majibu sahihi

K k d uk 101

SURA YA TANO

Ufahamu: shairi

Washirikishe wanafunzi katika kutaja baadhi ya vipingele muhimu vya ushairi

Toa maelezo mafupi kwa kila kipengele

www.arena.co.ke 0713779527

Mfano

Arudhi, tarbia, manju, kibwagizo

Wanafunzi walisome shairi kwa sauti

Waongoze wanafunzi kulichambua shairi kwa misingi ya arudhi za ushairi

Wajibu maswali

K k d uk 53-54

Kihusishi: ‘katika’ na kiambishi tamati ‘ni’

Katika hutumika kuonyesha uhusiano w kitu na mahali, huonyesha hasa ndani ya au kwenye

Mfano

Maji yamo katika chupa

Abiria wamo katika basi

Wanafunzi wamo katika darasa

Ni hutumika kuonyesha ndani ya au mahali ndani

Mfano

Vijiko vimo jikono

Walimu wamo majilisini

Mzazi yumo ofisini

Wajibu maswali

Kusikiliza na kuongea: misemo

Waambie wanafunzi wataje misemo yoyote wanayoifahamu

Wengine watoe maana ya misemo iliyotajwa

Waweke kwenye makundi ili waweze kujadili kuhusu misemo

Watoe majibu kwa kutamka

Mfano

Kumezea mate – kutamani

Kata rufani – kuomba kesi isikizwe upya

www.arena.co.ke 0713779527

Wahimize watumie misemo hiyo katika insha

Msamiati: aina za magari

Ni chombo cha kusafiria kiendacho kwa magurudumu

Tumia michoro ya magari kama nyenzo

Wanafunzi watazame picha na wataje majina ya aina ya magari

Jadiliana na wanafunzi majibu

Pikipiki – gari lenye magurudumu mawili na lenye mtambo

Rukwama –gari linalokokotwa na maksai na lenye magurudumu mawili bila mtambo

Kifaru – gari la chuma la kivita lenye mzinga

INSHA MUHULA WA PILI

HOTUBA

Hotuba ni maneno au malezo maaluma yanayotokana na mtu mmoja mbele ya hadhira

Anayetoa hotuba huitwa hatibu

Hadhira ni watu wanaohutubiwa

Hotuba inaweza kuwa ya

Mwalimu mkuu juu ya wazazi

Mwanasiasa nyakati za kampeni

Maafisa wa serikali katika sherehe tofauti

Rais akihutubia taifa

Mambo ya kuzingatia

Kufuata itifaki

Kutambua waliohidhuria kufuata cheo/mamlaka na umri

Mfano “mwalimu mkuu, naibu wa mwalimu mkuu, viranja na wanafunzi wenzangu jamjambo? _____

Wakati uliopo hutumika yaani usemi halisi

www.arena.co.ke 0713779527

Nafsi ya kwanza naya pili hutumika

Mfano

Nimesimama kadamnasi nikiwa mzima kama kigongo _____

Hutumia alama za kunukuuu ikiwa unahutubia kwa niaba ya mtu mwengine

Mfano

rais, naibu wa rais _____

Kila hoja husimuliwa katika aya yake

Hitimisho huhusu kuwashukuru wasikilizaji na pia kuwapa funzo au changa moto au nasaha

Umuhimu wa elimu

Elimu ni mafunzo yanayopatikana shulenina maishani

Hupevusha fikira

Mja hujielewa, huelewa wengine na ulimwengu

Huheshimiana

Huweza kutumia raslimali vilivyo

Elimu hundoa ujinga/ujuha

Mwanafunzi humakinika katika maisha ya vaadaye

Msamiati

Leo si jana ,jana si leo

Enda na ucheo, siende na uchwao

Elimu ya vitabu humsaidia mtu kuhifadhi siri ujumbe na kumbukumbu za kutumia na kizazi cha baadaye

Msamiati

Elimu huboresha maisha

Kujenga makao mazuri

Kuwasaidia jamaa na jamii

Elimu ni daraja la kuvusha mtu kwenye gange/kazi yenyefulusi nono

www.arena.co.ke 0713779527

Mtu hupata hela za kujimudu pasi kuwategemea wengine

Methali

Mtegemea cha nduguye hufa maskini

Mtegemea nundu haachi kunona

Mja hupewa heshima

Ragba

Nimesimama imara kama chuma cha pua

Tisti kama ngarange za mvule

Kidete kama kitawi cha mkarakala

Pongezi za dhati

Ninawapa mkono wa tahania kwa kufanya bidii za mchwa na duduvule

Nawamiminia shukrani sufufu

Ninawashukuru kwa kujitolea mhanga na kujifunga kibwebwe/masombo/kujikaza kisabuni

Methali

Elimu ni bahari

Elimu maisha si vitabu

Elimu ni taa gizani hung’aa

Elimu ni mali ambayo adui hawezi kuteka

Elimu bila mali kama nta bila asali

Tashbihi

Bidii za mchwa /duduvule

Ng’aa kama mbalamwezi

Pesa kama njugu

Julikana kama pesa

www.arena.co.ke 0713779527

Misemo

Kujito;ea mhanga

Shika usukani

Kuna kichwa

Ambua kitu

Tia pamba/nta

METHALI ZA KUTOHADAIKA NA UZURI WA NJE WA KITU NA TAMAA

Hutumiwa kuwaonya adinasi dhidi ya kudanganyika au kuhadaika na uzuri wa kitu bila kudadisi matokeo na athari zake

Methali ikiwa kama kichwa huhitajika kuelezea maana ya nje, ya ndani na matumizi

Mfano wa visa

Kumkaribisha mtu nyumbani

Kupatiwa lifti

Biashara gushi

Urembo

Fisadi

Methali

Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti

Hakuna kizuri kisichokuwa na dosari

Penye urembo ndipo penye ulimbo

Uzuri wa mkakasi, ukipata maji basi

Vyote ving’aavyo sio dhahabu

Tama ilimwua fisi

Uzuri si hoja hoja ni tabia

Mpanda farasi wawili hupasuka msamba

www.arena.co.ke 0713779527

Mtaka yote hukosa yote

Mbio za sakafuni huishia ukingoni

Mla kwa wawili hana mwisho mwema

Penye uhondo pana uvundo

Uzuri wa biyu ndani mabuu

Usiache mbachao kwa msala upitao

Vipokezi vya methali

Kwa yakini _____

Taib_____

Ama kweli_____

Kuntu_____

Ni jahara kama pengo kuwa _____

Ni wazi kama ju ala mtikati kuwa _____

Chambilecho wahenga au wazee wenye tabasuri tepetepe_____

Nahau

Maji kuzidi unga

Kitumbua kiliingia mchanga

Valia miwani

Meza mrututu

Meza mate machungu

Tulia huku ukitolea kule

Vimba kichwa

Kuwa na mkono mrefu

Bwaga zani

www.arena.co.ke 0713779527

Takriri

Dhahiri shahiri

Haambiliki hasemezeki

Hakanywi hakanyiki

Kuwa kiguu na njia

Hana harusi hana matanga

Ragba

Walimdekeza mwana wao

Alikuwa ndumakuwili aliyeuma ndani yakini kikulacho ki nguoni

Alijaribu bahati kwani asiyekuwa na bahati habahatishi

Pigwa kipopo

Temea mate

Kumwonea gere

Mambo yalimwendea sambejambe

Alilia kilio cha kite

Tashbihi

Huzunika kama mfiwa

Kuwa na wasiwasi kama mwasi

Aminika kama njiwa

Jambo wazi kama mchana

Kuwa mzembe kama kupe

MICHEZO

Ni jambo lifanywalo kwa ajili ya kujifurahisha kujichangamsha au kupoteza wakati

Baadhi ya michezo

www.arena.co.ke 0713779527

- Jugwe
- Gugwi
- Bembea
- Kibe
- Msabaka
- Kandanda
- Riadha
- Sarakasi
- Netiboli
- Naga
- Voliboli
- Gololi
- Hoki
- Langalanga
- Kriketi
- Mpira wa wavu
- Kandanda

Pia huitwa kambumbu, soka , gozi au mpira wa miguu

Hushirikisha timu mbikli pinzani

Wachezaji huvalia

- jezi
- Daluga
- Soksi
- Bukta

Katika ya uwanja huitwa kitovu/senta

Otea – kujificha kwa makusudi ya kushambulia kwa ghafla

Penalty – adhabu kwa mlindalango

Mlindalango, mdakaji, golikipa

Kimia

Refa/refarii

Mshika bendera/kibendera

Mhimili/goli

Ngware – cheza visivyo

Kipindi cha lala salama ni kipindi cha nwishi

www.arena.co.ke 0713779527

